# Nakala ya Wanafunzi ya Mambo Wanayopaswa na Wasiopaswa Kufanya Wanapotumia Maski

Fanya hivi unapovaa na kuvua maski yako.

Kabla ya kuvaa maski yako, nawa mikono yako kwa kutumia sabuni na maji au tumia sanitaiza iliyo darasani ili kusafisha mikono.

Maski yako inapaswa kutoshea vizuri kwenye mdomo na pua yako.

Ikiwa maski hiyo ina waya wa chuma, sogeza waya ili utoshee kwenye sehemu ya juu ya pua yako.

Ni muhimu kujaribu kutogusa maski yako wakati umeivaa. Ikiwa itabidi uirekebishe ili itoshee vizuri, tumia vitanzi vya sikio au kamba zilizo kwenye sehemu ya nyuma.

Ikiwa utagusa maski yako, safisha mikono yako au tumia sanitaisa iliyo darasani ili kusafisha mikono.

Unapovua maski yako, usiguse sehemu ya mbele. Vua maski yako kwa kutumia vitanzi ambavyo huzunguka masikioni mwako au kamba zinazozunguka kichwa chako.

Baada ya kuvua maski yako, nawa mikono yako au tumia sanitaiza ya kusafisha mikono mara moja.

Waulize walimu wako wakati sawa wa kuvua maski yako, kama wakati wa kupumzika au wakati wa kula.

Sikiliza walimu wako ili ujue ni wapi unapaswa kuweka maski yako ^wakati^unapoivua, ili kuiweka salama wakati hujaivaa.

Hakikisha umevaa maski safi shuleni kila siku.

Maski yangu inakulinda na maski yako inanilinda.

Tembelea health.mn.gov kwa maelezo yanayochipuka kuhusu COVID-19.

Minnesota Department of Health
Communications Office
P.O. Box 64975
St. Paul, MN 55164-0975
651-201-4989
health.communications@state.mn.us
www.health.state.mn.us

09/04/20
Mask Do's and Don'ts For Students (Swahili)
Ili kupata maelezo haya katika muundo tofauti, piga simu kwa: 651-201-4989.